

Kupatana tena kwa Familia: Wasiowakimbizi walio na Haki Kamili ya Kubakia

Maelezo yafuatayo yatakusaidia kukusanya maelezo mengi na ushahidi unaowezekana kabla ya kuja mbele ya mshauri wa kisheria au wakili ili kujadili kupatana tena kwa familia.

Iwapo una **Haki kamili ya kubakia** lakini wewe **sio mkimbizi** na ungependa mtu mmoja wa familia kuja na kuishi nawe katika Uingereza, utahitaji kuthbitisha yafuatayo:

- Kuwa una haki kamili ya kubakia. Kwa mfano Nyaraka ya Hali yako ya Uhamiaji.
- Kuwa wana uhusiano nawe. Kwa mfano ndoa, kuzaliwa/hati ya kulea, harusi au picha za familia.
- Kuwa unawasiliana nao mar akwa mara. Kwa mfano, kadi za simu, barua, risito za utumaji pesa.
- Kuwa wewe na familia yako mnaweza kuishi Uingereza bila kupokea pesa zaidi kutoka kwa faida ulizo nazo sasa. Kwa jumla, hii inamaanisha kuwa lazima uwe na nyuba kubwa ili kuweza kutoshea watu watakaojiunga kwa sababu ya kazi. Kwa mfano, taarifa za benki, mkataba wa kazi na hati za malipo, makubaliano ya upangaji wa nyumba au baru akutoka kwa mkabaila wako.

Mwanafamilia aliye ng'ambo lazima athibitishie Balozi wa Uingereza:

- 1) Katika hali ya mume/mke/mwenzi kiserikali¹ :
 - Kuwa wote pamoja nawe wana miaka 21 au zaidi.
 - Kuwa mmewahi kukutana na mna nia ya kuishi pamoja kama mke na mume, wenzi wa kiserikali, au kama wenzi² (pamoja na wa jinsia moja).
- 2) Katika hali ya mtoto (pamoja na aliyeasiliwa):
 - Kuwa yeye yuko chini ya miaka 18 na hajaolewa au kuishi peke yake.
 - Aitha:
 - o Wazazi wote wako Uingereza; au
 - o Wewe pekee unawajibika kwa utunzaji wana ulezi wa mtoto huyu (kwa kutuma pesa na kufanya uamuzi wa mambo muhimu au kwa kuwasiliana mara kwa mara na mtoto huyo).
- 3) Katika kesi ya jamaa wengine:
 - Kuwa wao ni wazazi wako au babu/bibi; mtoto, dada, ndugu, shangazi, au mjomba; na
 - Iwapo sio mzazi au babu/bibi juu ya miaka 65 na kuwa wanaisha pekee yao katika hali za kurumiwa zaidi³ kwa mfano kuugua ugonjwa au umasikini na kutoweza kufanya kazi bila wewe; na
 - Kuwa wanakutegemea kifedha; na
 - Kuwa hakuna jamaa wengine walio karibu ili kuwasaidia.

1 Utambuzi wa kisheria wa uhusiano wa kati ya jinsia moja

2 Wenzi ambao hawajaoana lazima wawe katika uhusiano wa ndoa kwa miaka 2

3 Sheria za Uhamiaji, aya 317

Maelezo mengine muhimu

- Nyaraka zingine za asili zitafsiriwe kwa Kiingereza
- Iwapo mtu wa familia yako ana pasi ya kusaifiri au nyaraka ya kutambulishwa inaweza kuwa msaada mkubwa kwa ombi lako.
- Wainaishi katika hali gani kwa sasa? Na nani? Ni nani huwasaidia? Kwanini hawawezi kuishi nao tena?

Onyo: Pesa za kutoa ombi lazoma zilipwe kwa balozi wa Uingereza ng'ambo

Maelezo muhimu unaoweza kukusanya ili kufuata masharti

Yanayohitajika kuhusu Masharti	Mifano ya Ushahidi
Haki Kamili ya Kubakia	Nyaraka ya hali yako ya uhamiaji Nyaraka yako ya usafiri
Uhusiano/sehemu ya familia	Hati ya ndoa Hati ya kuzaliwa/kuasiliwa ya mtoto Picha za ndoa au za familia
Kuwasilana kwa mara	Kadi za simu au kumbukumbu Barua Risiti za ubadilishaji wa fedha
Pesa za usaidizi wa kutosha	Mkatoba wa kazi Hati za malipo Taarifa za benki
Makazi yanayofaa	Makubaliano ya upangaji nyumba Barua kutoka kwa mkabaila

Ni nani anaweza kusaidia?

Halmashuri ya Wakibizi ya Uskoti huwa haitoa huduma ya upatanaji tena wa familia. Hata hivyo, mwakilishi wako wa kisheria anaweza kukusaidia. Iwapo huna mmoja au ungependa kubadilisha mwakilishi wako, tunaweza kukupa majina na anwani ya wawakilishi wa kisheria.

Kama ilivyowekwa juu, iwapo ungependa kujua kuhusu hili, tafadhali hakikisha kuwa umezingatia mahitaji na ushahidi unaofaa ambao utahusika kabla ya kutuma ombi.



Scottish Refugee Council 5 Cadogan Square,
(170 Blythswood Court) Glasgow G2 7PH
Ushauri wa bure wa simu: 0800 085 6087
Barua pepe: info@scottishrefugeecouncil.org.uk
Wavuti: www.scottishrefugeecouncil.org.uk
Ufadhili Uliosajiliwa Nambari: SC008639

